BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Sita – Tarehe 26 Septemba, 2018.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2017/2018.

Wizara ya Afya:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Afya ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2017/2018.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii Kuhusu Ripoti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2017/2018.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii Kuhusu Ripoti ya Wizara ya Afya ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2017/2018.

II. MASWALI:

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

146. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

Wananchi wa Zanzibar wengi hawafahamu Taasisi za Muungano, majukumu yake na vipi Zanzibar inavyofaidika.

(a) Je, kwanini Taasisi za Muungano wanakuwa wazito kutoa elimu kwa wananchi kuhusu majukumu yao na Zanzibar inavyonufaika na kusababisha upotoshaji mkubwa kujitokeza kutoka kwa baadhi ya wanasiasa.

(b) Je, Serikali ya Mapinduzi inanufaika na gawio la kiasi gani kwa mwaka katika Taasisi za Muungano.

(c) Je, kuna Taasisi na Mashirika mangapi ya Muungano yanayofanya kazi na Zanzibar.

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

58. MHESHIMIWA SHEHE HAMAD MATTAR (Jimbo la Mgogoni) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Kwa kuwa Ofisi ya Wakfu na Mali ya Amana ilikuwa na jengo la zamani la Wakfu hapo Chake Chake-Pemba. Na kwa kuwa Afisi ya Wakfu ilitiliana mkataba na mfanyabiashara wa hapo Chake Chake kufanya ujenzi wa Afisi za Wakfu pamoja na milango ya biashara na kujilipa kwa njia ya kodi.

(a) Je, hadi sasa mfanyabiashara huyo ameshajilipa kiasi gani.

(b) Je, ni baada ya muda gani mjenzi huyo atakuwa tayari ameshajilipa.

(c) Je, jengo hilo liligharimu kiasi gani.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

101. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Hivi karibuni kumefanyika operesheni ya kuvunja maduka na sehemu za biashara katika maeneo mbali mbali ya Manispaa za Mjini. Hali hiyo imeleta taharuki na fadhaa kwa wafanyabiashara wengi ambao hawajafanya matayarisho ya kutosha ya kuhamisha biashara zao wakati operesheni hiyo inafanyika.

(a) Je, kwanini Serikali haitoi notisi mapema kuwajulisha wafanyabiashara hao kabla ya kuchukuwa hatua za kuvunja.

(b) Kumekuwa na mtindo wa wananchi kuachiwa wajenge majengo yao mpaka wamalize na kuhamia ndipo baadae Serikali huja na wazo la kuvunja, Je, kwanini hatua hazichukuliwi tokea mapema kabla mwanachi hajaanza ujenzi.

103. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Kwa nia nzuri tu Serikali imewahamisha wafanyabiashara wa mbao eneo la Kijangwani kupisha ujenzi wa kituo kipya cha Daladala kwa Manispaa ya Mjini. Hata hivyo muda mrefu umepita kituo hicho bado hakijaanza kazi mbali na kuwekwa kifusi na kujengwa choo.

(a) Je, Kituo hicho lini hasa kitaanza kazi.

(b) Je, kiasi gani cha gharama zimetumika kuweka kifusi na kujenga choo katika eneo hilo.

Wizara ya Elimu Na Mafunzo ya Amali:

65. MHESHIMIWA SAID OMAR SAID (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Tarehe 10/2/2018, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein, kupitia mkutano wa Chama cha Walimu Zanzibar, alielekeza Wizara ya Elimu kumaliza madeni ya walimu na kukaa na chama hicho kutatua changamoto za elimu Zanzibar. Kauli hiyo aliirejea katika maadhimisho ya Mei Mosi Wete, Pemba tarehe 01/05/2018.

(a) Je, Wizara imefikia hatua gani katika utekelezaji wa maagizo hayo.

(b) Je, kuna mafanikio na changamoto gani zilizojitokeza katika hatua zinazochukuliwa na Wizara.

Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto:

60. MHESHIMIWA SAADA RAMADHAN MWENDWA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto:

Kwa muda mrefu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikitoa mikopo kwa vikundi mbali mbali vya wanawake wa Mjini na Vijijini. Hata hivyo, kiwango cha mikopo hiyo ni kidogo sana na hakiwezi kupunguza umaskini kwa wananchi hao.

(a) Je, Wizara ina mpango gani kwa mwaka 2018/2019 kuongeza kiwango cha mikopo hiyo.

(b) Je, ni vikundi vingapi vya wanawake wa Mikoa wa Mjini Magharibi ambavyo vilifaidika na mikopo hiyo kwa mwaka 2017/2018.

(c) Je ni kiasi gani cha fedha kilichotumika kutoa mikopo kwa wanawake wote wa Zanzibar kwa mwaka 2017/2018.

Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo:

121. MHESHIMIWA SULEIMAN SARHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo:

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa juhudi zake za ujenzi wa viwanja vya michezo. Hata hivyo, suala la umiliki wa viwanja hivyo bado halijakaa sawa ikiwemo uwanja wa Gombani ya Kale, Tibirinzi pamoja na uwanja wa Gombani.

(a) Je, Kiwanja cha Gombani ya Kale na kiwanja cha Tibirinzi vinamilikiwa na nani.

(b) Je, kiwanja cha Gombani kimepimwa na kina hati miliki.

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzuia viwanja hivyo ili kuhakikisha havivamiwi.

Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

31. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

Kwa kuwa Kamisheni ya Ardhi ni moja kati ya taasisi muhimu sana ambayo imekabidhiwa kupanga kazi ya usimamizi wa utawala wa ardhi na matumizi bora ya ardhi.

(a) Je, Idara ya Upimaji na Mipango Miji ili kuweza kufanyakazi zake kikamilifu, inahitaji wafanyakazi wangapi wenye utaalamu wa kufanya tathmini ya ardhi na majengo sambamba na wataalamu wa kupanga miji.

(b) Je, ni changamoto gani inayoikabili Idara ya Upimaji na kusababisha baadhi ya watu kujenga bila ya kufuata utaratibu wa mipango miji na kuweza kuleta athari kubwa ya kimazingira hapo baadae.

III. HOJA ZA SERIKALI:

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

Ripoti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2017/2018.

Wizara ya Afya:

Ripoti ya Wizara ya Afya ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2017/2018.

Zanzibar,
26 Septemba, 2018.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.